HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI CHA TAREHE 14/02/2024

KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA COMMUNITY CENTRE

MAHUDHURIO

A. WAJUMBE

| NA. | JINA | | CHEO | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pancras | Maliyatabu | -Mwenyekiti wa Halmashauri | -Mwenyekiti |
| 2. | Ndg William | Mwakalambile | - Mkurugenzi Mtendaji (W) | -Katibu |
| 3. | Mhe.Stephen | Kayogolo | -Makamu Mwenyekiti H/W | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Egid | Ngomeni | -Diwani Kata ya Nkomolo | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mpemba | Evarist | - Diwani Kata ya Nkandasi | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dismas | Msangawale | -Diwani Kata ya Kate | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. Badwin | Mathew | -Diwani Kata ya Mashete | -Mjumbe |
| 8. | Mhe. Maria | Ndauka | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Namanyere | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. Osward | Kamsipi | -Diwani Kata ya Kizumbi | -Mjumbe |
| 10. | Mhe. Muhamad | Zaid | -Diwani Kata ya Mkinga | -Mjumbe |
| 11. | Mhe. Vitalis | Malipesa | -Diwani Kata ya Korongwe | -Mjumbe |
| 12. | Mhe. Janeth | Kashamakula | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 13. | Mhe. Emiliana | Kauzeni | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kate | -Mjumbe |
| 14. | Mhe. Magreth | Maembe | -Diwani Viti Maalum Tarafa yaNamanyere | -Mjumbe |
| 15. | Mhe. Wensesikaus | Kapita | -Diwani Kata ya Ninde | -Mjumbe |
| 16. | Mhe. Robert | Kasongo | -Diwani Kata ya Mkwamba | -Mjumbe |
| 17. | Mhe. Nestory | Kaloto | -Diwani Kata ya Namanyere | -Mjumbe |
| 18. | Mhe. Godfrid | Bendera | -Diwani Kata ya Majengo | -Mjumbe |
| 19. | Mhe. Garincha | Kiliko | -Diwani Kata ya Itete | -Mjumbe |
| 20. | Mhe. Joseph | Mwenda | -Diwani Kata ya Kipande | -Mjumbe |
| 21. | Mhe. Francis | Nkoswe | -Diwani Kata ya Ntuchi | -Mjumbe |
| 22. | Mhe. Kakuli | Seba | -Diwani Kata ya Kirando | -Mjumbe |
| 23. | Mhe. Mohamed | Adam | -Diwani Kata ya Kipili | -Mjumbe |
| 24. | Mhe. Frank | Mtakwita | -Diwani Kata ya Wapembe | -Mjumbe |
| 25. | Mhe. Gerald | Kalikisha | -Diwani Kata ya Sintali | -Mjumbe |
| 26. | Mhe. Karolina | Makandi | -Diwani Kata ya Paramawe | -Mjumbe |
| 27. | Mhe. George | Saninga | -Diwani Kata ya Myula | -Mjumbe |
| 28. | Mhe. Roswita | Sululu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 29. | Mhe. Ruteghata | Miambi | -Diwani Viti Maalum Tara ya Chala | -Mjumbe |
| 30. | Mhe. Kudra | Ahamed | -Diwani Kata ya Kipundu | -Mjumbe |
| 31. | Mhe. Isaack | Chambula | -Diwani Kata ya Isunta | -Mjumbe |
| 32. | Mhe. Masai | Leonard | -Diwani Kata ya Ntatumbika | -Mjumbe |
| 33. | Mhe. Privatus | Yolam | -Diwani Kata ya Kala | -Mjumbe |
| 34. | Mhe. Michael | Mwanalinze | -Diwani Kata ya Chala | -Mjumbe |
| 35. | Mhe. Anastazia | Kasagama | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kirando | -Mjumbe |
| 36. | Mhe. Priska | Mbeyu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Chala | -Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

| NA. | JINA | | CHEO | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Aida | Khenani | -Mbunge Nkasi Kaskazini | -Kwa Taarifa |
| 2. | Mhe. Vicent | Mbogo | -Mbunge Nkasi Kusini | - Kwa Taarifa |

**B. WATAALAM**

| NA. | JINA | | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg Valeriana | Mwapasi | Afisa Mali asili na Mazingira (W) |
| 2. | Ndg Mayuma | Nzilantuzu | Afisa Mazingira na Udhibiti TakNgumu (W) |
| 3. | Dr John | Tlatlaa | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 4. | Ndg Nicodemas | Hillu | Afisa Ardhi (W) |
| 5. | Ndg lucia | Mwami | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 6. | Ndg Emmanuel | Gamasa | Kaimu Afisa Kilimo, Takwimu na Ufuatiliaji (W) |
| 7. | Ndg Richard | Katyega | Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu (W |
| 8. | Ndg Marietha | Mwanisenga | Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 9. | Ndg Nsubisi | Mwakasege | Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W) |
| 10. | Ndg Apotunas | Mussi | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 11. | Ndg Justina | Mwita | Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi (W) |
| 12. | Ndg Steward | Vidoga | Kaimu Afisa Mipango na Uratibu (W) |
| 13. | Ndg Rashid | Masoud | KaimuAfisa Mtendaji Mkuu Mamlaka Mji Mdogo Namanyere |
| 14. | Ndg Abas | Kiroge | Kaimu Mkaguzi wa Ndani |
| 15. | Ndg Kelvin | Toyi | Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 16. | Ndg Fred | Kisoko | Kaimu Mweka Hazina |
| 17. | Eng Gido | Monji | Kaimu Mhandisi Wa Ujenzi |
| 18. | Ndg Didas | Sadani | Kaimu Mwanasheri wa Halmashauri |
| 19. | Ndg John | Ntulo | Kaimu Afisa TEHAMA (W |
| 20. | Ndg Patrick | Kipesha | Mwandishi wa Vikao |

**C. MAAFISA TARAFA**

| NA. | JINA | | CHEO | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ndg Diana | Khan | -Afisa Tarafa | Chala |
| 2. | Ndg Kasimu. | Ibrahim | -Afisa Tarafa | Namanyere |
| 3. | Ndg Revocatus | Chikala | -Kaimu Afisa Tarafa | Kirando |
| 4. | Ndg Erasto. | Widambe | -Kaimu Afisa Tarafa | Wampembe |
| 5. | Ndg Misheck | Chapewa | -Kaimu Afisa Tarafa | Kate |

**D. WAGENI WAALIKWA**

| NA | JINA | | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg Lumara | Madirisha | Kaimu Meneja TARURA(W) |
| 2. | Ndg Thomas | Petro | Kaimu Meneja RUWASA |

**E. WAANDISHI WA HABARI**

| NA. | JINA | | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg Israel | Mwaisaka | - Mtangazaji Nkasi FM |
| 2. | Ndg Pet[illegible] | Siame | -Mwandishi wa Habari TBC |
| 3. | Ndg Baraka Lusajo | | -Mwandishi wa Habari ITV |

**AGENDA.NA.NKS/DC/BRZ/01/02/2024**
**KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe wataalam, wageni waalikwa, na wananchi waliohudhuria Baraza, kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili kufungua kikao.
Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 5:45 asubuhi.

**AGENDA.NA.NKS/DC/ BRZ /02/02/2024**
**KUTHIBISHA AGENDA**

Wajumbe walithibitisha agenda

**AGENDA.NA.NKS/DC/ BRZ /03/02/2024**
**KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA**

Mwenyekiti aliwapitisha wajumbe ukurasa kwa ukurasa wa muhtasari na kufanya marekebisho. Wajumbe waliridhia muhtasari usainiwe kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao kilichopita.

**AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /04/02/2024**
**KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA TAASISI ZA SERIKALI ROBO YA PILI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

A. TARURA

Kaimu Meneja TARURA(W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/24. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Mjumbe alitaka kujua barabara zilizo mbovu katika vijiji mbalimbali ni lini zitaanza kurekebishwa
-Mjumbe alitaka kujua kutokana na mvua nyingi kunyesha barabara nyingi zimeharibika ni lini zitaanza kurekebishwa ili kurahisisha usafiri kwa wananchi kutokana na barabara nyingi kujifunga
-Mjumbe Mwingine alitaka kujua Mkandarasi aliyepewa kurekebisha barabara ya Namanyere kakoma ni lini atasambaza vifusi vilivyomwagwa barabarani kwani imekuwa kero kwa wananchi
- Mjumbe mwingine alipongeza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kwa kazi nzuri wanazozifanya hasa kuhakikisha barabara mbalimbali zinakarabatiwa sasa ni vyema kuanza kuona kufunga barabara mbalimbali zilizojifunga
-Mjumbe âliomba Wakara wa barabara Mjini na Vijijini(TARURA) kuomba bajeti ya ziada kutokana na barabara zilizo nyingi kuharibika kutokana na mvua nyingi

. Baada ya michango hiyo Kaimu Meneja TARURA alipokea shukrani na kuwahakikishia waheshimiwa Madiwani kuwa barabara zote zilizo mbovu zinaendelea kufanyiwa ukarabati kadri fedha zinavyotolewa na wizara, hivyo barabara zote zitafikiwa, kuhusu kuomba bajeti wizara imeashaliona suala hilo kuna bajeti ya dharura inakuja kwa ajili ya barabara zote zitakazoharibika hasa kipindi hiki cha mvua kubwa zinazonyesha. Baada ya majibu hayo Wajumbe walipokea taarifa na kuunga mkono hoja.

B. RUWASA

Kaimu Meneja RUWASA (W)-Nkasi aliwasilisha taarifa ya majukumu na kazi mbalimbali zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/24. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Mjumbe alitaka kujua katika bajeti waliyowasilisha eneo la Mashete wataalam walitembelea na wakaweka makisio ya gharama, katika bajeti waliyowasilisha haikuwekwa ni lini mradi huo utatengewa fedha

-Mjumbe alitaka kujua taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zilizounganishwa kwa kipindi cha robo ya pili. Baada ya michango ya Wajumbe Meneja wa RUWASA alipokea ushauri na kujibu baadhi ya hoja kuwa kwa robo ya pili RUWASA imeunganisha zaidi ya Taasisi 18 kuhusu Mashete ipo katika Bajeti inayokuja. Wajumbe walipokea taarifa na kuunga mkono hoja

**AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /05/02/2024**

**KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA KATA ROBO YA PILI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

Wajumbe waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Kata ambapo taarifa za Kata zifuatazo ziliwasilishwa; Kata ya *Chala, Isale, Ntuchi, Isunta, Itete, Kabwe, Kala, Kate, Kipande, Kipili, Kipundu, Kirando, Kizumbi, Korongwe, Majengo, Mashete, Mkinga, Mkwamba, Mtenga, Myula, Namanyere, Ninde, Nkandasi, Nkomolo, Ntatumbila, Paramawe, Sintali* na *Wampembe.* Baada ya kuwasilisha taarifa wajumbe walipata nafasi ya kuchangia kama ifuatavyo. -

- Mjumbe aliashauri taarifa za kata zipite katika vikao vya Kata (WDC) kwani huko hujadiliwa kwa kina
- Mjumbe alihoji mpango mkakati wa Halmashauri katika kukusanya mapato ya ndani kutokana na utoroshaji wa mapato katika kata kuwa mkubwa na Watendaji hawafuatilii ukusanyaji wa mapato
- Mjumbe mwingine aliomba Halmashauri kupitia mapato ya ndani kuweka mkakati mathubuti wa kuanza kumalizia maboma mbalimbali ambayo yalishaanzishwa na Wananchi
- Mjumbe alishauri Katika taarifa za makusanyo kuna kata zimekusanya vizuri sana na zingine zimekusanya kidogo ni vyema zile zilizokusanya kidogo zijifunze kwa walioweza
- Wajumbe walishauri Mashine za kukusanyia Mapato (POS Mashine) zinunuliwe kutokana na vituo vingi kukosa mapato hayo.
- Pia Wajumbe walishauri ili kuweza kufikia lengo katika ukusanyaji wa mapato hasa ukanda wa ziwa Tanganyika Mkurugenzi Mtendaji aweke mikakati mathubuti ya kukusanya katika eneo hilo.
- Mjumbe aliomba mashine za boti zilizokwisha nunuliwa na kupelekwa ukanda wa mwambao isimamiwe ipasavyo ili kuweza kukusanya mapato ya Halmashauri isiwe wamepelekewa watu kwa shughuli zao binafsi.
- Mjumbe mwingine alishauri leseni za uvuvi zikusanywe kwa wakati ili kuinua kipato cha Halmashauri.

Baada ya hoja za wajumbe Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwapongeza wajumbe kwa kuwasilisha taarifa za kata, na kuwahakikishia wajumbe kuwa ushauri na mikakati yote iliyozungumzwa hasa upande wa ukusanyaji wa mapato utazingatiwa ili kuweza kuongeza mapato ya Halmashauri

Baada ya hapo Wajumbe waliunga mkono hoja.

AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /06/02/2024

KUFUNGA KIKAO

Katibu aliwapongeza wajumbe kwa michango yenye tija kwa maendeleo ya Halmashauri, na alipokea ushauri uliotolewa na kuahidi maagizo na maelekezo yatazingatiwa, kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa uwasilishaji wa taarifa pamoja na maoni yao, pia alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji (W) pamoja na Wakuu wa Idara na vitengo kwa ufafanuzi na akasisitiza maagizo yaliyotolewa yatekelezwe.

Kikao kilifungwa saa 10:15 jioni

MUHTASARIUMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA

| | |
|---|---|
| ………………………………… | ………………………………… |
| WILLIAM MWAKALAMBILE | MHE.PANCRAS MALIYATABU |
| KATIBU | MWENYEKITI |

Tarehe 31/05/2024

HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI CHA TAREHE 15/02/2024

KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA COMMUNITY CENTRE

MAHUDHURIO

A. WAJUMBE

| NA. | JINA | | CHEO | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pancras | Maliyatabu | -Mwenyekiti wa Halmashauri | -Mwenyekiti |
| 2. | William | Mwakalambile | -Mkurugenzi Mtendaji (W) | -Katibu |
| 3. | Mhe.Stephen | Kayogolo | -Makamu Mwenyekiti H/W | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Egid | Ngomeni | -Diwani Kata ya Nkomolo | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mpemba | Evarist | - Diwani Kata ya Nkandasi | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dismas | Msangawale | -Diwani Kata ya Kate | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. Badwin | Mathew | -Diwani Kata ya Mashete | -Mjumbe |
| 8. | Mhe. Maria | Ndauka | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Namanyere | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. Osward | Kamsipi | -Diwani Kata ya Kizumbi | -Mjumbe |
| 10. | Mhe. Muhamad | Zaid | -Diwani Kata ya Mkinga | -Mjumbe |
| 11. | Mhe. Vitalis | Malipesa | -Diwani Kata ya Korongwe | -Mjumbe |
| 12. | Mhe. Janeth | Kashamakula | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | –Mjumbe |
| 13. | Mhe. Emiliana | Kauzeni | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kate | -Mjumbe |
| 14. | Mhe. Magreth | Maembe | -Diwani Viti Maalum Tarafa yaNamanyere | -Mjumbe |
| 15. | Mhe. Wensensilaus | Kapita | -Diwani Kata ya Ninde | -Mjumbe |
| 16. | Mhe. Robert | Kasongo | -Diwani Kata ya Mkwamba | -Mjumbe |
| 17. | Mhe. Nestory | Kaloto | -Diwani Kata ya Namanyere | -Mjumbe |
| 18. | Mhe. Godfrid | Bendera | -Diwani Kata ya Majengo | -Mjumbe |
| 19. | Mhe. Garincha | Kiliko | -Diwani Kata ya Itete | -Mjumbe |
| 20. | Mhe. Joseph | Mwenda | -Diwani Kata ya Kipande | -Mjumbe |
| 21. | Mhe. Francis | Nkoswe | -Diwani Kata ya Ntuchi | -Mjumbe |
| 22. | Mhe. Kakuli | Seba | -Diwani Kata ya Kirando | -Mjumbe |
| 23. | Mhe. Mohamed | Adam | -Diwani Kata ya Kipili | -Mjumbe |
| 24. | Mhe. Frank | Mtakwita | -Diwani Kata ya Wapembe | -Mjumbe |
| 25. | Mhe. Gerald | Kalikisha | -Diwani Kata ya Sintali | -Mjumbe |
| 26. | Mhe. Karolina | Makandi | -Diwani Kata ya Paramawe | -Mjumbe |
| 27. | Mhe. George | Saninga | -Diwani Kata ya Myula | -Mjumbe |
| 28. | Mhe. Roswita | Sululu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 29. | Mhe. Ruteghafa | Miambi | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Chala | -Mjumbe |
| 30. | Mhe. Kudra | Ahamed | -Diwani Kata ya Kipundu | -Mjumbe |
| 31. | Mhe. Isaack | Chambula | -Diwani Kata ya Isunta | -Mjumbe |
| 32. | Mhe. Masai | Leonard | -Diwani Kata ya Ntatumbika | -Mjumbe |
| 33. | Mhe. Privatus | Yolam | -Diwani Kata ya Kala | -Mjumbe |
| 34. | Mhe. Michael | Mwanalinze | -Diwani Kata ya Chala | -Mjumbe |
| 35. | Mhe. Anastazia | Kasagama | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kirando | -Mjumbe |
| 36. | Mhe. Priska | Mbeyu | Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kate | -Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Mhe. Aida | Khenani | -Mbunge Nkasi Kaskazini | -Kwa Taarifa |
| 2. Mhe. Vicent | Mbogo | -Mbunge Nkasi Kusini | -Kwa Taarifa |

**B. WATAALAM**

| NA. JINA | | CHEO |
|---|---|---|
| 1. Ndg Valeriana | Mwapasi | Afisa Mali asili na Mazingira (W) |
| 2. Ndg Mayuma | Nzilantuzu | Afisa Mazingira na Udhibiti TakNgumu (W) |
| 3. Dr John | Tlatlaa | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 4. Ndg Ladslaus | Mzelela | Afisa Kilimo, Takwimu na Ufuatiliaji (W) |
| 5. Ndg Nsubisi | Mwakasege | Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W) |
| 6. Ndg Richard | Katyega | Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu (W |
| 7. Ndg Marietha | Mwanisenga | Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 8. Ndg Lucia | Mwani | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 9. Ndg Nestory | White | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 10. Ndg Justina | Mwita | Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi (W) |
| 11. Ndg Atufigwege | Mwakitega | Kaimu Afisa Mipango na Uratibu (W) |
| 12. Ndg Rashid | Masoud | KaimuAfisa Mtendaji Mkuu Mamlaka Mji Mdogo Namanyere |
| 13. Ndg Salu | Makoye | Kaimu Mkaguzi wa Ndani |
| 14. Dr Makundi | Mazige | Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 15. Ndg James | Mwanisawa | Kaimu Mweka Hazina |
| 16. Eng Gido | Monji | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi |
| 17. Ndg Didas | Sadani | Kaimu Mwanasheri wa Halmashauri |
| 18. Ndg John | Ntulo | Kaimu Afisa TEHAMA (W |
| 19. Ndg Patrick | Kipesha | Mwandishi wa Vikao |

**C. MAAFISA TARAFA**

| NA. JINA | | CHEO | |
|---|---|---|---|
| **1.** Ndg Diana | Khan | -Afisa Tarafa | Chala |
| **2.** Ndg Kasimu. | Ibrahim | -Afisa Tarafa | Namanyere |
| **3.** Ndg Revocatus | Chikala | -Kaimu Afisa Tarafa | Kirando |
| **4.** Ndg Erasto. | Widambe | -Kaimu Afisa Tarafa | Wampembe |
| **5.** Ndg Misheck | Chapewa | -Kaimu Afisa Tarafa | Kate |

**D. WAANDISHI WA HABARI**

| NA. JINA | | CHEO |
|---|---|---|
| **1.** Ndg Israel | Mwaisaka | - Mtangazaji Nkasi FM |
| **2.** Ndg Pety | Siame | -Mwandishi wa Habari TBC |
| **3.** Ndg Baraka | Lusajo | -Mwandishi wa Habari ITV |

AGENDA. NA. NKS/DC/BRZ/01/01/2024

KUFUNGUA KIKAO

Katibu aliwakaribisha wajumbe, wataalam, wageni waalikwa na wananchi waliohudhuri katika Baraza la madiwani la kujadili taarifa za robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua kikao.

Mwenyekiti alizingatia itifaki, kisha aliwasihi wajumbe kuzingatia kanuni wakati wa uendeshaji wa kikao. alifungua kikao saa 5:30 asubuhi.

AGENDA. NA. NKS/DC/BRZ/02/02/2024

KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA

Mwenyekiti aliwapitisha wajumbe ukurasa kwa ukurasa wa muhtasari na marekebisho yalifanyika. Wajumbe waliridhia muhtasari usainiwe kama kumbukumbu sahihi ya kikao kilichopita.

AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /03/02/2024

MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MHESHIMIWA MWENYEKITI WA HALMASHAURI NA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

Katika kikao hiki hakukuwa na maswali ya papo kwa papo kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) wala kwa Mwenyekiti wa Halmashauri

AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /04/02/2024

TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA PILI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

A. : TAARIFA YA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa. Wajumbe walipokea na kuchangia kama ifuatavyo:

-Mjumbe alipongeza kamati kwa kuliona suala la kondom kusambazwa katika maeneo mbalimbali hasa vijijini kutokana na wananchi wanaoishi huko kuwa na uelewa mdogo juu ya ugonjwa wa Ukimwi ni vyema pamoja na kusambaza kondom hizo elimu itolewe vya kutosha kuhusu matumizi ya kondom hizo

Mjumbe mwingine alipongeza wajumbe wa kamati kushauri asasi mbalimbali zinazojishughulisha na mapambano dhidi ya virusi vya UKIMWI kuunganisha nguvu kwa pamoja ili kupambana na janga hili

**Mwenyekiti wa Kamati** aliwashukuru wajumbe kwa pongezi na kuahidi kuendelea kusimamia Halmashauri na asasi kwa ujumla kuweza kutekeleza majukumu yao.

B. : TAARIFA YA KAMATI YA ELIMU NA AFYA

Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu na Afya aliwasilisha taarifa mbele ya wajumbe. Wajumbe walipokea na kuchangia kama ifuatavyo: -

-Mjumbe alipongeza kamati kwa kuliona suala la ukamilishaji wa maboma katika shule za Msingi, Sekondari na Zahanati ni vyema jambo hili likawekewa mkakati mzuri ili kuweza kuwapa wananchi moyo pale walipotoa nguvu zao

-Mjumbe mwingine alishauri kuendelea kusimamia Halmashauri kuhakikisha ukarabati wa nyumba za walimu zilizochakaa ili walimu waishi katika mazingira mazuri na waweze kufanya kazi kwa moyo

**Mwenyekiti wa Kamati** aliwashukuru wajumbe kwa michango na ushauri uliotolewa na kuahidi kuwasimamia wataalam kutekeleza maagizo yaliyotolewa.

## C. TAARIFA YA KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa. Wajumbe walipokea na kuchangia kama ifuatavyo: -

-Wajumbe walipongeza kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kwa kuliona suala la utoaji wa elimu juu ya matumizi ya mbolea inayoletwa kwani kwa sasa mbolea zimeletwa aina tofauti tofauti wananchi wanashindwa kujua ipi ni bora na ipi sio bora

-Mjumbe mwingine aliomba kamati iendelee kusimamia ukamilishaji wa majosho ya Ntalamila, Chalatila na Kate ili yakamilike kwani ni muhimu sana katika kuogesha mifugo

**Mwenyekiti wa Kamati** aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na alishauri Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kutekeleza maazimio ya kamati. pomoja na ushauri uliotolewa.

## D. TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango aliwasilisha taarifa. Wajumbe walipokea na kuchangia kama ifuatavyo;

-Wajumbe walipongeza kamati kwa kujadili mambo ya msingi na walishauri mikakati mbalimbali juu ya ukusanyaji wa mapato iwekwe ili kufikia lengo liliiokusudiwa

-Mjumbe alisisitiza maboti yaliyonunuliwa na kupelekwa ukanda wa mwambao mwa ziwa Tanganyika yatunzwe na kufanya kazi iliyokusudiwa

**Mwenyekiti wa Kamati** aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuahidi kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kuendelea kuisimamia Halmashauri ili kuweza kuongeza mapato.

## AGENDA. NA.NKS/DC/ BRZ /05/02/2024
## KUFUNGA KIKAO

Katibu alimpongeza Mwenyekiti wa Halmashauri kwa kuongoza kikao vizuri na kuahidi maagizo mbalimbali yaliyotolewa yatazingatiwa na kufanyia kazi

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalam na vingozi wote kwa uvumilivu na kuwa wasikivu Kikao kilifungwa saa 8: 20 mchana

MUHTASARI
UMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA

| | |
|---|---|
| ……………………… | ……………………… |
| William Mwakalambile | Mhe Pancras Maliyatabu |
| KATIBU | MWENYEKITI |

Tarehe 01/06/2024